Mpingo Conservation & Development Initiative

MCDI Misitu ya Jamii Tanzania-Uthibitishaji wa Pamoja

SD06 Taratibu za Kiusalama msituni

Version 1.0 – 09/12/11

Huduma ya Kwanza

Ni muhimu Sanduku la Huduma ya kwanza likawepo wakati wa shughuli zote za msituni kwa sababu ili kukabiliana na majeruhi yanapotokea. Pia kwa sababu misitu ipo mbali na huduma za afya kama vile Zahanati ni vyema huduma ya kwanza ikawepo karibu.

Sanduku la huduma ya kwanza linatakiwa kuwa na vitu vifuatavyo:

- Pamba
- Antiseptic solution
- Adhesive plaster
- Bandaji
- Spirit
- Tincture iodine
- Crepe bandages
- Gloves
- Mshumaa na kibiriti
- Gentian violet
- Kijitabu cha kuweka kumbukumbu

Dawa za kuvuia maumivu hazitakiwi kuwepo kwenye sanduku la huduma ya kwanza. Hii ni kwa ajili ya kuzuia matumizi yasiyo sahihi ya dawa ambayoyanaweza kusababisha watu kujizidishia dawa.

Mambo muhimu yafuatayo ni lazima yazingatiwe:

- Sanduku lazima liandikwe "SANDUKU LA HUDUMA YA KWANZA" na liwekwe vitu vinavyohusiana na Huduma ya Kwanza tu.
- Mameneja wa Msitu wachague mtu mmjoja aliyefuzu mafunzo ya Huduma ya Kwanza ili kusimamia utoaji wa Huduma ya kwanza. Jina la mtoa Huduma ya Kwanza liwepo ndani ya sanduku la Huduma ya Kwanza.
- Msimamizi wa Uvunaji ahakikishe kuwa Sanduku la Huduma ya Kwanza lina vitu vyote vinavyotakiwa kabla ya kuanza uvunaji.

Taratibu za kufuata wakati wa tukio la majeruhi au ajali

1. Matukio yote ya majeruhi ni lazima yawasilishwe kwa msimamizi wa uvunaji mara moja.
2. Msimamizi wa Uvunaji au mtu yeyote aliyepata mafunzo ya kutoa huduma ya kwanza atatoa huduma ya kwanza kwa majeruhi.
3. Usafiri ni lazima uwepo wakati uvunaji ili kupeleka majeruhi kwa huduma zaidi inapotokea ajali.
4. Kwa matukio ya kawaida, majeruhi watapelekwa katika zahanati ya Kijiji. Kwa matukio makubwa kama vile kuvunjika mfupa majeruhi wapelekwe Hospitali ya Wilaya. Wavunaji wote ni lazima wawe na Bima ya Afya ya Taifa.
5. Athari zozote zitakazotokea katika msitu wa hifadhi kwa mfano mtu kujeruhiwa taarifa lazima itolewe kwa meneja wa umoja ndani ya siku 30 kwa kutumia fomu *SF11 Taarifa ya Majeruhi.*
6. Kama ilivyobainishwa katika Sheria ya Usalama kazini ya mwaka 2003, taarifa za matukio yote ya ajali ziwasilishwe kwa mwakilishi wa mkaguzi mkuu wa viwanda (au Afisa Kazi wa Wilaya) ndani ya masaa 24 na taarifa ya maandishi iliyojazwa kwenye fomu ya serikali iwasilishwe ndani ya kipindi cha siku saba.
7. Meneja wa Umoja ataweka kumbukumbu zote za taarifa za majeruhi katika fomu EF09. Orodha ya taarifa za majeruhi. Baada ya tukio meneja wa umoja atawasiliana na msimamizi wa uvunaji na kujaza fomu ya tathmini ya athari kwa kutumia fomu EF15. Meneja wa umoja atatoa ushauri kwa ajili ya kuzuia matukio hayo kwa siku zijazo na kuwapa taarifa wanachama wote na wasimamizi wa uvunaji.

Taratibu za kulipa fidia

Kwa sasa wanajamii wote ambao watapata majeraha msituni watafidiwa na Serikali za Vijiji vyao kutokana na malipo yaliyopatikana kwa kuuza rasilimali za msitu. Halmashauri ya Kijiji itakaa na kujadili kiwango sahihi cha fidia. Mameneja wa misitu wanaweza kuwasiliana na Meneja wa Umoja ili kuomba ushauri katika kupanga kiasi cha fidia. Fidia italipwa kwa kuzingatia viwango vya fidia vya Serikali.

Kama inawezekana fidia inaweza kutolewa toka vyanzo vya mapato vilivyopo la sivyo Mameneja wa Misitu watalipa fidia watakapoanza kupata mapato ya mazao ya misitu. Kama hili likijitokeza ulipaji fidia ni lazima upewe kipaumbele dhidi ya matumizi mengine. Hili linaweza kusababisha kuchelewa kuanza kwa mipango mingini ya matumizi ya pesa.

Endapo mtu aliyepata majeraha na kufidiwa hakuridhika na kiwango cha fidia wanaweza kutoa malalamiko yao kwa Meneja wa Umoja. *Rejea SD08: Taratibu za Kutoa Malalamiko na Kukata Rufaa.*

Usimamizi wa Moto

Moto ni kitu cha hatari sana katika usimamizi wa misitu hasa miombo. Moto huhatarishi misitu na unaweza kuathiri ukuaji wa miti na mambo mengine ya kiasili. Hapa tutaangalia zaidi madhara ya moto kwa wanaofanya kazi msituni.

Kuzuia moto kichaa

Wakati wa shughuli za msituni, ni vyema watu wakachukua taadhari juu ya mahali moto hutokea hasa kipindi cha kiangazi. Kama ukigundua moto kichaa unakuja upande wako ni lazima uondoke maeneo hayo mara moja. Angalia mwelekeo wa upepo. Mioto mingi inaweza kuepukika kwa njia hii. Ukiwa nyuma ya moto hapo ni salama hasa ukiwa umezungukwa na maeneo ambayo tayari yameshaungua moto.

Kama haiwezekani kuukimbia moto, kimbilia kwenye gari au nenda eneo salama ambalo lina kinga za moto au mahali salama kama vile juu ya kichuguu. Hili ni eneo ambalo lina nyasi chache kavu au nyasi mbichi nyingi ambazo haziwezi kuungua. Unaweza pia kusafisha nyasi kavu zinazokuzunguka. Moto ukikukaribia uzime kwa kutumia mafukutu mabichi. Wakati umezungukwa na moto jaribu kuinama ili kuzuia moshi na kupata hewa safi chinichini.

Mtu yeyote aliyeadhirika na moto ni lazima apewe huduma ya kwanza haraka iwezekanavyo.

Kutumia moto kama chombo cha Usimamizi misitu

Wakati wa kutumia moto kama chombo cha Usimamizi kama vile kubabua, taratibu zifuatazo ni lazima zifuatwe:

- Chagua eneo ndani ya msitu ambalo halikuungua mwaka uliopita.
- Anza kwa kuwasha moto mdogo katika eneo ulilolithibiti
- Usichome au kubabua Eneo ambalo halitavunwa
- Zima moto kwa kutumia matawi na mafukutu ukianza kwenda zaidi ya eneo ulilokusudia.
- Usichome karibu na miti yenye mazalia au viota vya ndege.

Mafunzo

Mafunzo ya Huduma ya Kwanza yatatolewa kwa baadhi ya wanajamii watakaosimamia Huduma ya Kwanza. Mafunzo yatatolewa na Shirika la Msalaba Mwekundu (TRCS) na yanaweza kutolewa na Mtalaam wa shirika la mpingo aliyefuzu mafunzo ya Ufundishaji Huduma ya kwanza.

Mafunzi ya Huduma ya kwanza yatajumuisha yafuatayo;

- Jinsi ya kutoa Huduma ya Kwanza
- Kuzuia ajali
- Kutoa taarifa za majeruhi au ajali
- Maandalinzi ya dharura na majanga
- Utunzaji mazingira
- Kukabiliana na dharura na majanga
- Sanduku la Huduma ya kwanza na vifaa vyake
- Kuboresha afya ya wanajamii.
- Mafunzo kwa vitendo ya namana ya kutoa Huduma ya kwanza.

Mwisho wa mafunzo, washiriki watafanya mtihani na kupatiwa vyeti vya kufuzu.

Mafunzo ya UKIMWI yanaweza kutolewa na mtaalamu wa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya au toka shirika la msalaba mwekundu.